

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI ZANZIBAR

08/09/2023

TAARIFA KWA UMMA JUU YA BEI ZA MAFUTA KWA MWEZI SEPTEMBER 2023.

Mamlaka ya Udhubiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) inatangaza Bei za Mafuta kwa Mwezi wa Septemba 2023. Bei hizo zitaanza kutumika rasmi Siku ya Jumamosi Tarehe 09/09/2023.

Mamlaka hupanga bei kwa kuzingatia mambo yafuatayo:

- Wastani wa mwenendo wa mabadiliko ya bei za mafuta Duniani (Platts Quatations).
- Gharama za uingizaji Mafuta katika Bandari ya Dar-es-Salaam na Tanga.
- Thamani ya Shilingi ya Tanzania kwa Dola za Kimarekani.
- Gharama za Usafiri, Bima na 'Premium' hadi Zanzibar.
- Kodi na Tozo za Serikali.
- Kiwango cha faida kwa Wauzaji wa Jumla na Reja Reja.

Bei za mafuta kwa Septemba 2023 ni kama zifuatazo:

AINA YA MAFUTA	BEI YA MWEZI AGOSTI, 2023 (TZS/LITA)	BEI YA MWEZI SEPTEMBER, 2023 (TZS/LITA)	TOFAUTI (TZS/LITA)	TOFAUTI ASILIMIA (%)
PETROLI	2,970	2,950	-20	-0.67
DIZELI	2,843	3,012	169	5.94
MAFUTA YA TAA	2,921	2,921	-	-
MAFUTA YA NDEGE	2,365	2,448	83	3.51

Sababu za kuongezeka Bei za Dizeli na Mafuta ya Ndege ni kuongezeka Bei hizo katika soko la Dunia kwa asilimia 21 na gharama za bima na usafirishaji kwa asilimia 62 ikilinganishwa na Mwezi Agosti.

Mamlaka inawahimiza Wananchi kununua Mafuta katika Vituo halali vya Mafuta na kudai Risiti za Kielektroniki kila wanaponunua Mafuta.

IMETOLEWA NA KITENGO CHA UHUSIANO (ZURA)

